# ZIJUE HAKI ZA WANAWAKE TANZANIA



# ZIJUE HAKI ZA WANAWAKE TANZANIA

# ZIJUE HAKI ZA WANAWAKE TANZANIA

## WALIOSHIRIKI KATIKA WARSHA YA UANDISHI NA UHARIRI WA KITABU HIKI NI:-

1. Asseny Muro — Ofisi ya Waziri Mkuu
2. Jane Kikopa — Wizara ya Biashara na Viwanda
3. Mwajuma Mponji — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
4. Rustica Chengelela — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
5. Ellen Binagi — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
6. -Suzan Kayetta — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
7. Mary Rusimbi — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
8. Stella Shayo — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

Pia wafuatao walitoa mchango wao kwa kusoma mswada wa awali na kutoa mapendekezo.

1. Ndugu T.F. Ngalula — Chuo cha Ustawi wa Jamii Dar es Salaam
2. Ndugu A.G. Bubeshi — Wizara ya Sheria

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
P.O. Box 20679,
Dar es Salaam.

© Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima 1984.

Picha zimechorwa na B. Ngwawasya

Printed in Tanzania by

# YALIYOMO


Ukurasa

1. **Dibaji** .......................................... v
2. **Utangulizi** .......................................... vi
3. **Sura ya Kwanza:**
   Haki za Wanawake katika ndoa .................. 1
4. **Sura ya pili:**
   Haki za Wanawake katika Elimu ................ 9
5. **Sura ya Tatu:**
   Haki za Wanawake katika kumiliki Ardhi ......... 14
6. **Sura ya Nne:**
   Haki za Wanawake kushirikishwa katika Uongozi .............................. 22
7. **Sura ya Tano:**
   Haki za Wanawake katika Malezi .............. 29

# DIBAJI

Ni muhimu kwa kila raia kuelewa haki zake katika jamii na pale anaponyimwa haki kudai. Kitabu hiki 'Zijue Haki za Wanawake Tanzania' kinachambua haki za wanawake katika nyanja za kilimo, elimu, sheria na ajira kwa madhumuni ya kuwafanya wanawake kuzielewa na hatimaye kuzidai endapo watakosewa haki. Aidha, kitabu hiki kitasaidia kukuza uwezo wa wanawake katika kusoma na kuandika, hasa kwa wale waliokwishafuzu kisomo chenye manufaa. Mwisho, kitabu hiki kitawapa wanawake msukumo wa kuendelea siku hata siku kupigania haki zao hadi ushindi kamili wa kujenga usawa kati ya wanaume na wanawake katika jamii utakapopatikana.

Napenda kutoa shukrani kwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa hatua waliyoichukua kuandika kitabu hiki. Ni mchango mkubwa katika maendeleo ya wanawake Tanzania. Pia, shukrani nazitoa kwa waandishi waliojitokeza kuandika mada mbali mbali katika kitabu hiki. Shukrani pia ziwaendee wale wote kwa njia moja au nyingine wameshiriki katika kufanikisha uandaaji wa kitabu hiki.

Ni matumaini yangu kuwa wanawake walio wengi watakisoma na kutafakari yale yote yaliyomo kwenye kitabu hiki kwa manufaa yao na kwa manufaa ya jamii kwa ujumla. Mwisho natoa wito kwa wanaume kukisoma hiki kitabu ili waweze kushirikiana na wanawake katika kulinda haki zao.

Ndugu G. Mongela (Mb)
Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu

## UTANGULIZI

Nafasi ya mwanamke katika ujenzi wa Taifa imetiliwa mkazo katika nchi yetu ya Tanzania. Mwanamke analo jukumu na anastahili nafasi kubwa katika maendeleo yake. Kwa hivyo, kuna umuhimu wa kumpa mwangaza wa kujua mambo yote yanayomhusu.

Madhumuni ya kitabu hiki ni kumpa changamoto na kumwelimisha mwanamke wa Kitanzania kutambua nafasi, majukumu na haki zake katika jamii. Kimeandikwa kwa lugha nyepesi na kwa kutumia vielelezo vingi ili kumwelimisha msomaji kutambua masuala muhimu juu ya ndoa, elimu, malezi, maendeleo na uongozi kwa ujumla.

Tunatumaini kwamba, yote yaliyomo yatawafikia walengwa na kuiamsha ari ili wawe na hamu ya kuzijua haki za wanawake na uwezo wao wa kushiriki kikamilifu katika kupigania usawa na haki za binadamu wote kwa maendeleo ya Taifa.

**WAANDISHI**

# SURA 1

## HAKI ZA WANAWAKE KATIKA NDOA

Tumepata kulisikia neno ndoa mara nyingi na ingefaa tuliangalie maana yake. Kwa misingi ya sheria ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanamke na mwanamume unaotarajiwa uwe wa kudumu maisha yao yote. Baada ya kufunga ndoa wahusika hupaswa kuishi pamoja. Uamuzi wa kuishi pamoja ni wa kufa na kupona, raha au taabu, kupata au kukosa na kuchuma kwa matumizi ya wote katika nyumba.

## AINA ZA NDOA

Nchini Tanzania kuna aina tatu za ndoa ambazo zimekubaliwa chini ya misingi ya Sheria ya Ndoa ya 1971. Aina hizo ni Kimila, Kidini na Kiserikali. Kwa kuwa ndoa hizi zinafungwa katika mazingira ya Kiafrika, mila na desturi nyingine ziambatanazo na ndoa bado zinaendelea. Mathalani, idhini ya wazazi wa pande zote mbili, mahari, na mambo mengine mengi ya kimila bado yanafanyika ingawa hutofautiana kufuatana na kabila.

Kuhusu suala la mahari, yamekuwepo mabishano mengi, baadhi ya watu wakidai yasiwepo kabisa na wengine wakidai yawepo isipokuwa yawekewe kiwango kisheria. Hata hivyo, hakuna ufumbuzi kamili uliofikiwa kuhusu suala hili. Badala yake wanaohusika wameachiwa wajiamulie wenyewe. Hata hivyo, Sheria inasema kuwa, ndoa isikataliwe kufungwa kwa sababu tu ya kutolipa mahari; endapo mahari itabaki, ichukuliwe kama deni la kawaida. Lakini, mtindo wa baadhi ya makabila kudai kulipwa mahari kabla ya ndoa imekuwa ni kikwazo kwa wanawake katika kudai haki zao kwenye ndoa.

Watu wanapoingia katika maisha ya ndoa huwa wanaanza maisha mapya kabisa wakiwa na mategemeo

makubwa baadaye. Matarajio yao ni kushirikiana kwa kila wanachokipata au kuchuma, kusaidiana shida zinapotokea na kuyakabili matatizo ya wazazi wa pande zote mbili. Pia inawabidi wajiandae kupokea familia yao pindi watakapojaliwa kupata watoto na kuwatunza watoto hawa kwa imani na upendo.



Wazazi ni walezi wa familia.

## HAKI NA WAJIBU KATIKA NDOA

Kisheria, mume anawajibika amtunze mkewe kwa kadiri ya uwezo wake. Matunzo yenyewe ni kama kumpa mavazi, chakula, na huduma nyingine za muhimu. Endapo mume atakataa kwa makusudi kumtunza mke wake, sheria inaruhusu mwanamke huyu kupata amri ya matumizi kutoka mahakamani itakayomlazimisha mumewe kumtunza. Hali ya matunzo itategemea uwezo wa kiuchumi alionao mwanamume huyo. Pia mke anawajibika kumtunza mumewe endapo mume huyo hajiwezi kutokana na maradhi ya mwili au akili. Kama wapo watoto na ndugu wengine wanaoishi hapo ni wajibu wa mwanamume vile vile kuwatunza.

Hata hivyo, mke anayo ruhusa ya kuuza mali yoyote ya mumewe au hata kwa jina la mumewe ili apate matumizi yake na wanae iwapo mumewe ana uwezo wa kumtunza lakini hafanyi hivyo. Kwa sababu hii, anaweza akauza mali au vitu vya mume wake kama vile nguo, viatu, redio, vitabu, saa na vifaa vingine ili mradi apate fedha za matumizi ya familia. Iwapo mume ana gari au baisikeli mke anaweza akaviweka rehani vitu hivyo ili apate fedha. Hii inawezekana wakati mume na mke wanaishi pamoja au kama wamekubaliana kuishi mbalimbali lakini mume akimtunza.

Ingawa mwanamume ana wajibu mkubwa katika utunzaji wa familia, ingefaa sana kama mume na mke wangeshirikiana kupanga mahitaji pamoja na makadirio ya matumizi kwa ajili ya mahitaji ya familia. Mipango thabiti itapunguza matatizo ya ugomvi kuhusu fedha na matumizi.

Wanawake ndio watunzaji wa familia na hivyo watunzaji wa ghala za chakula. Iko tabia ya mmojawapo kuuza mazao yote ya chakula, pamoja na mboga na matunda. Hii huleta athari mbaya na hatimaye mafarakano au hata kuvunjika kwa ndoa.

## MALI KATIKA NDOA

Mwanamke aliyeolewa anahaki na uwezo wa kuwa na mali yake binafsi bila kuingiliwa na mume wake. Kwa mara ya kwanza mwanamke anapata haki ya kumiliki mali anayoichuma mwenyewe kutokana na shughuli zake mbalimbali. Tangu zamani iliaminika kwamba, mwanamke akiolewa shughuli zote azifanyazo anamfanyia mume wake, lakini sasa mwanamke aliyeolewa anaweza kununua mali au ardhi kutokana na ruzuku ya kazi yake. Hata kama alikuwa na mali yoyote kabla ya kuolewa, mali hiyo ni yake. Hivyo, mwanamke asishurutishwe kuiandikisha mali yake katika jina la mume wake, endapo yeye hataki kufanya hivyo.

Ni hivi majuzi tu shughuli za mwanamke na juhudi zake za nyumbani zimetambuliwa kama mchango mkubwa katika kuchuma mali ya familia. Hii imempa haki za kugawana mali iliyochumwa wakati wa maisha ya ndoa. Mwanamke pia anao uwezo wa kuingia katika mkataba wowote kwa mfano mikataba ya kukopa, kununua vitu, kupata huduma, n.k. na anayo haki ya kushtaki au kushtakiwa endapo makubaliano ya mkataba hayazingatiwi.

Mara nyingi mke na mume wakiishi pamoja wanasaidiana katika shughuli kwa mfano za kujenga nyumba. Hali kadhalika hushirikiana kununua vitu mbalimbali ambavyo huwekwa kwa jina la pamoja au la mume tu. Mali yote hiyo kisheria ni yao pamoja na kama ikibidi kuachana, wakati wa talaka watagawana mali hiyo.

Katika mila za Kiafrika, mwanamke akiolewa hujiona kwamba amefikia mwisho wa kujishughulisha na mambo yanayomhusu binafsi. Hii sivyo. Mwanamke yeyote hana budi kujishughulisha na kujiendeleza katika mambo ya kila siku. Inampasa ajifunze kusoma na kujiendeleza; pia ajishughulishe na michezo, ajiunge kwenye vyama na kuhudhuria mikutano mbalimbali.

## MATATIZO KATIKA NDOA

Maisha katika ndoa hayana budi yaambatane na haki za binadamu. Tunaamini binadamu wote ni sawa na wanastahili haki sawa. Lakini, inaonekana kwamba, kushindwa kwa maisha ya ndoa aghalabu kunaletwa na kutomjali mwanamke na hivyo kudhalilisha utu wake. Matatizo ya ndoa huletwa na kuvunja makubaliano ya mkataba wa ndoa kwa namna moja au nyingine. Migogoro mingi hutokea, mmojawapo anapokuwa hakidhi haja za mwenzake au za familia kwa ujumla. Vile vile, matatizo hutokea katika ndoa endapo mume au mke atakuwa mlaghai kwa kutumia pesa ovyo kwa mfano katika ulevi, uasherati au matumizi mengine mabaya na ya kibinafsi na kwa namna hii kuitesa familia yake. Ingawa wanawake wengi ni wavumilivu, vituko vikizidi kupita kiasi, ustahimilivu wao hufikia kikomo. Kwa namna hii migogoro midogo hukua hadi kufikia kupigana, kutengana au kuachana. Hali kama hii inapotokea, amani hukosekana na mara nyingi wanaopata shida ni watoto kwa sababu huweza kukosa malezi bora ya baba na mama.

Ni jambo la kusikitisha sana kuwa mpaka sasa bado kuna wanawake wengine wanaoonewa na kunyanyaswa sana na waume zao, na huvumilia tu kwa kuwa bado hawajajua haki zao.

## KUVUNJIKA KWA NDOA

Ugomvi au kutoelewana huweza kutokea katika maisha ya ndoa. Hii hutegemea aina ya ugomvi na kwamba kutoelewana huko hutokana na nini. Zamani kabla ya Sheria ya ndoa ya mwaka 1971 watu wakichukizana au kugombana waliweza kwenda mahakamani kutaka talaka bila hata kutafuta usuluhishi na kujua kosa ni nini au ni la nani. Kwa namna hii mwanamke hakuwa na haki ya kuuliza kwa nini afukuzwe na hata kudai haki zake nyingine.




Utaratibu uliopo kisheria ni kwamba, kabla mtu hajapeleka maombi ya kutaka talaka ni lazima aende kwenye baraza la usuluhishi wa ndoa. Hii ni katika kuwashauri na kujaribu kupatanisha mke na mume ikiwa kumezuka ugomvi au kutoelewana kati yao. Endapo baraza litashindwa kusuluhisha, barua itatolewa ambayo mwomba talaka ataambatanisha ndipo talaka itolewe. Vinginevyo talaka haiwezi kutolewa. Zaidi ya haya mwombaji pia atawajibika kuthibitisha kuwa ndoa yake imevunjika kiasi ambacho haiwezi kutengenezeka.


Wakati ndoa inapofungwa haitegemewi kwamba itavunjika hapo baadaye. Lakini endapo itavunjika kutokana na matatizo mbalimbali basi mwanamke anazo haki fulani. Kwa mfano, mwanamke anayo haki ya kugawiwa mali iliyochumwa wakati wa maisha ya ndoa. Halikadhalika, mwanamke anayo haki ya kupewa watoto wake ili awalee.

Hapa sheria inamuruhusu mwanamke kukaa na watoto walio chini ya umri wa miaka saba. Hata hivyo, mahakama ina uwezo wa kuamua ni mzazi yupi akae na watoto ili waweze kulelewa vizuri kiafya na kitabia.

## KIFO

Ndoa ikivunjika kutokana na kifo cha mume, mke hubaki akiwa mjane. Kutokana na hali hii, ni lazima afikirie namna ya kuendelea kuishi kwa kujitegemea. Na kama anao watoto itabidi aendelee kuwalea.

Katika hali hii, wakati wa kuamua mambo ya mirathi, mwanamke ni lazima apewe haki kurithi mali ya mume wake.



Mama huyu ameshikwa na majonzi ya kufukuzwa katika nyumba baada ya mume wake kufariki.

Katika makabila mengi, mwanamke hunyang'anywa mali hii eti kwa kuwa hana haki ya kuwa mrithi. Hii si kweli, bali inatokana na hali ya kumwonea mwanamke.

Baada ya mume kufariki, mwanamke anao uhuru wa kuamua kurithiwa na ndugu wa mume wake au kubaki hivi hivi bila kuolewa. Mara nyingi mwanamke hufikiriwa kwamba yeye ni chombo kwa hiyo ni lazima arithiwe la sivyo wazazi wake warudishe mahari.

Haki katika ndoa ni nyingi na mwanamke akizijua ataweza kuendesha maisha yake akiwa na mwelekeo. Si vizuri mtu kuonewa au kunyanyaswa kana kwamba hana utu wake. Kuzijua haki za wanawake kutasaidia kutatua matatizo mengi katika ndoa.

# SURA YA PILI

## HAKI ZA WANAWAKE KATIKA ELIMU

Elimu ni tendo lolote la kujifunza ambalo humwongezea binadamu ujuzi na maarifa ambayo atayatumia kubadili mazingira yake. Kujifunza kusoma na kuandika kwa mfano, kutamsaidia mtu kuweza kuelewa maandishi mbalimbali kama vile kusoma maagizo ya dawa kutoka kwa daktari au maelekezo ya utumiaji bora wa mbolea na kadhalika. Mtu huyo pia atakuwa na uwezo wa kujieleza kwa njia ya maandishi kama vile kuandika barua au kumbukumbu anazozihitaji kwa maendeleo yake na ya jamii kwa ujumla.

Kutokana na umuhimu huo, mwaka 1948 Umoja wa Mataifa ulipitisha haki ya kila binadamu kupata elimu. Binadamu wote duniani maskini au tajiri wana haki sawa katika maisha yao. Azimio hilo lilifungua usawa wa wanawake na wanaume katika kupata elimu. Tendo hili linathibitisha umuhimu wa elimu katika maisha ya binadamu kwani elimu ni ufunguo wa maisha. Kuna aina tatu za elimu nazo ni elimu ya jadi kama vile jando na unyago, elimu itolewayo mashuleni na elimu itolewayo nje ya shule. Lengo kubwa la elimu ni kumkomboa binadamu kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni.

Nchi nyingi zimetambua umuhimu wa elimu katika jamii na jitihada zinafanyika ili watu wote waipate. Akisisitiza juu ya umuhimu huo, Dr. Aggrey wa Ghana alisema kwamba ukimwelimisha mwanaume umemwelimisha mtu mmoja lakini ukimwelimisha mwanamke umeelimisha familia nzima. Hivyo tunaona wazi kwamba, ili kuleta maendeleo katika jamii, wanawake wana haki ya kupata elimu kwani watasaidia kuelimisha familia zao.

Historia inaonyesha kwamba suala la wanawake kupata elimu ulimwenguni kote lilipuuzwa. Hapa nchini Tanzania wakati wa ukoloni, elimu ya wanawake haikutiliwa maanani.

Hata ile elimu ya darasani iliyotolewa kwa wakati huo ilikuwa ya kibaguzi kwani ilitolewa kwa watu wachache kufuatana na rangi na dini zao. Isitoshe uandikishaji wa watoto katika madarasa ulipewa uzito zaidi kwa wavulana. Si hayo tu, bali pia baadhi ya wazazi hawakupenda hata baada ya Uhuru. Vile vile Serikali nayo ilitoa nafasi zaidi kwa wanaume. Hivyo matokeo yakawa asilimia kubwa zaidi ilikuwa ya wanaume wenye elimu ya juu zaidi. Ingawaje haja ya kuwaelimisha wasichana ilizidi kuongezeka mwaka hadi mwaka, ila wengi hawajui kusoma na kuandika jambo ambalo linawafanya washindwe kufahamu haki zao. Ni wajibu wa kila mwanamke kujielimisha kadri ya uwezo wake jambo ambalo litawafanya watu wote wa familia yake wapende kujiendeleza.

Baada ya uhuru, Serikali ya Tanzania ilifanya mapinduzi kwa kufutilia mbali tabaka zilizokuwepo kielimu na kupanua nafasi za elimu kwa wasichana na wavulana. Pamoja na jitihada hizo, wasichana walioipata elimu hiyo walikuwa ni wachache sana. Wananchi wengi mijini na vijijini hawakupata elimu hii ya darasani. Ili kuharakisha maendeleo ya nchi Chama na Serikali vinahimiza juhudi za kupiga vita dhidi ya maadui ujinga, maradhi na umaskini.

Rais J.K. Nyerere alitangaza mwaka 1970 kuwa ni mwaka wa Elimu ya Watu Wazima. Kila Mtanzania alipewa jukumu la kujiendeleza kadri ya uwezo wake kwa wakati wote wa uhai wake kwani elimu haina mwisho. Tamko hilo lilileta sura mpya ya Elimu ya Watu Wazima kwani Wizara ya Elimu ilipewa jukumu hilo, ndipo Idara ya Elimu ya Watu Wazima ilipoanzishwa kwa madhumuni hayo. Elimu watakayoipata itawasaidia wanawake kushiriki kwa ukamilifu katika kupanga, kutekeleza na kutathmini miradi yao, kwani imedhihirika kwamba, wanawake hushirikishwa katika utekelezaji tu na siyo katika upangaji. Hali hii imeonekana sana katika kampeni za kitaifa kama vile *Mtu ni Afya, Chakula ni Uhai* na miradi mbali mbali ya uchumi.

Wanawake wa Kitanzania hasa waishio vijijini wana haki ya kupata elimu kutokana na mchango wao mkubwa katika maendeleo ya taifa. Maendeleo vijijini hutegemea kilimo kwa kiwango kikubwa. Watu wanaohusika zaidi na kilimo vijijini ni wanawake ambao hubidi walime mazao mengi kwa ajili ya chakula na ziada ya kuuza ili kujipatia fedha za matumizi mabalimbali ya nyumbani. Kutokana na hali hii, ni muhimu wanawake wapate elimu ili juhudi zao katika kilimo na hata shughuli nyingine ziweze kuwa bora na za mafanikio zaidi.

Vilevile, ni muhimu wanawake wapewe nafasi nyingi zaidi za mafunzo mbalimbali ambayo huendeshwa vijijini, kitaifa au nchi za nje kwa njia ya semina, warsha, n.k. Vilevile katika mashindano ya kijiji bora wanawake wapewe nafasi kubwa. Mara nyingi mashindano hayo yamekuwa yakifanywa na wanaume tu. Halikadhalika, watu ambao wamekuwa wakiteuliwa kwenda katika safari fupi za mafunzo nje ya nchi wengi wamekuwa ni wanaume. Hali hii haina budi kubadilika na badala yake kuwapa wanawake nafasi zaidi za mafunzo ya ndani na nje ya nchi ambayo yatawaelimisha na kuwapa nafasi ya kuona maendeleo ya watu wengine duniani.

Wanawake wana haki ya kupatiwa elimu sasa kwa sababu zifuatazo: Kwanza, kutokana na jukumu lao katika jamii kama warithishaji mila kutoka kizazi hadi kizazi. Iwapo watapewa elimu ya kutosha, ni wazi kwamba upeo wao wa kurithisha mila na utamaduni wetu utakuwa mpana na wa kimapinduzi.

Pili, ni jambo linalojulikana wazi kwamba wanawake wameachwa nyuma kielimu kwa miaka mingi. Kwa vile ambavyo hali hii imebainika na umuhimu wa wanawake kuelimishwa umeonekana, ni haki kwamba wanawake wapewe nafasi nyingi zaidi za kuelimishwa na za mafunzo ili pengo lililopo kielimu kati ya wanawake na wanaume lizibwe.

Tatu kutokana na jukumu lao zito la uzalishaji mali vijijini, ni haki wanawake wapewe elimu ili mali

wanayozalisha iwe bora zaidi na nyingi. Ni dhahiri kwamba iwapo wanawake wataelimishwa kulingana na mazingira yao wataelewa zaidi na kuleta ufanisi kwa namna hii.

Nne, wanawake ndio walezi wa jamii zetu. Iwapo watapewa elimu hususa inayohusu malezi bora ya watoto ni dhahiri kwamba watalea watoto na jamii vizuri na kwa namna hii taifa litakuwa na maendeleo na wananchi wenye afya nzuri na nguvu za kulijenga taifa lao.

Tano, nchi nyingi duniani hivi sasa zinajitahidi kupiga vita ujinga. Nchi yetu nayo haikubaki nyuma katika jitihada hii. Ni muhimu kusisitiza kwamba, kwa kuwa wananchi walio wengi ni wanawake, kuwaelimisha na kuwapa nafasi za mafunzo kwa wingi, kutapunguza tatizo la kufuta ujinga kwa kiasi kikubwa. Hivyo, ili kuharakisha maendeleo ya taifa ni muhimu kuelimisha wanawake ambao kwa muda mrefu wamepuuzwa na kunyanyaswa.

Katika harakati za kutoa elimu kwa wote, imeonekana kuna matatizo ambayo yanawafanya wanawake wasinufaike na huduma hizi. Baadhi ya mila na desturi zetu huwafanya wanawake kutopata nafasi ya kuhudhuria masomo yanayotolewa kwani wengi wao hutindikiwa na shughuli za uzalishaji mali pamoja na shughuli za nyumbani-kama vile kupika, kuteka maji, kuokota kuni na shughuli nyingine. Mara nyingi kazi hizi humwacha mwanamke katika hali ya uchovu wa kimwili na kiakili. Hali hii humfanya hata akihudhuria masomo ya Elimu ya Watu Wazima asiweze kushiriki kikamilifu. Hivyo, sharti juhudi zifanywe ili kumpunguzia mwanamke mzigo huo kwa kutumia teknolojia.

Mtazamo wa wanawake na jamii kielimu pia ni tatizo. Watu wengine hawaoni umuhimu wa wanawake kupata nafasi ya kuelimishwa. Kwa mtazamo wao, wanaume tu ndio wenye haki ya kupata elimu. Baadhi ya wanawake pia hukubaliana na mtazamo huo kwani, hadi hivi leo masomo ya fani ya sanaa huchukuliwa na wanawake wakiogopa,

kuchukua masomo ya fani za sayansi, uhandisi n.k. Wanawake sharti wajikomboe kutokana na fikra hizo za kikale na wafanye kazi kwa kadri ya uwezo wao.

Tatizo jingine ambalo linaathiri utekelezaji wa elimu ya Watu Wazima ni ukosefu wa sheria inayosisitiza umuhimu wa wanawake kushiriki katika mipango ya elimu ya watu wazima. Kutokana na umuhimu wa mchango wao katika ujenzi wa taifa sharti elimu ya watu wazima itiliwe mkazo. Elimu hiyo itasaidia harakati za ukombozi wa taifa letu kifikra, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kiteknolojia.

# SURA YA TATU

## HAKI ZA AKINA MAMA KATIKA KUMILIKI ARDHI

Kwanza, akina mama vijijini ndio uti wa mgongo wa sekta ya kilimo. Ukweli huu unatambuliwa kitaifa. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alipokuwa anatangaza Azimio la Arusha mwaka 1967 alisema hadharani kwamba, akina mama vijijini wanafanya kazi kushinda akina baba. Hivyo, taifa linatambua kwamba wanawake wanashiriki kikamilifu katika kilimo.

Pili, kwa sababu mwanamke ni sawa na mtu mwingine yeyote, kwa hiyo ana haki ya kumiliki maliasili kuu ya Taifa-ARDHI. Tanzania inaamini katika usawa wa binadamu na kwamba kumnyima mama kijijini haki ya kumiliki ardhi ni kwenda kinyume cha imani yetu.

Tatu, kwa sababu wanawake hushiriki bega kwa bega na akina baba vijijini katika jitihada za kuleta mapinduzi ya kilimo Tanzania.



Picha: Akina mama wakilima shambani.

Ni wazi kwamba wanawake hawatashiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo vijijini kama hawatakuwa na haki ya kumiliki ardhi.

Kwa hiyo, ni nia ya sehemu hii kutamka wazi kwa akina mama vijijini kuwa, wanayo haki ya kumiliki ardhi na katika sehemu ambayo bado wanawake hawajawa na haki kama hiyo wanahitaji kudai haki hiyo sasa.


Pamoja na kutetea haki hii, wanawake watetea haki ya kumiliki mazao wanayolima, zana za kilimo, kuwa wanachama wa ushirika wa wakulima na kupata mikopo itakayowawezesha kuendeleza kilimo. Kumiliki au kujenga nyumba, kufuga na kumiliki mifugo.




Picha: Wanawake wakienda kuuza mazao yao katika ushirika wa wakulima.

## Historia ya Umilikaji Ardhi Tanzania

Katika vijiji vya Tanzania ardhi ndiyo msingi wa uzalishaji mali. Kabla ya kufika kwa wakoloni, babu zetu walijitegemea kwa mazao ya chakula kwa kutumia ardhi. Wakoloni walipofika walitumia ardhi yetu kupata utajiri mkubwa kutokana na mazao ya biashara (pamba, katani, kahawa, karanga na chai). Wakati wa ukoloni haki ya kumiliki ardhi ndiyo ilimpa mtu haki ya kuwa mwanachama katika vyama vya wakulima, kupata mikopo, hata haki ya kutumia mifereji kwa kumwagilia mashamba.



Picha: Mkulima kwenye shamba la kahawa.

**Mifano ya umilikaji Ardhi katika Vijiji kabla ya Ukoloni na kabla ya Azimio la Arusha.**

**Jamii ya Wasambaa:**

Familia ya Kisambaa ilikuwa na baba ambaye ndiye aliyekuwa kiongozi wa nyumba, mke (au wake) na watoto. Familia au jamii ilikuwa na aina mbili za ardhi. Kwanza, ardhi ya baba ambayo ilikuwa yake mwenyewe. Pili, ardhi ya wanawake ambayo walikatiwa vipande. Wake wa mtu walifanya kazi katika vipande vya mashamba siyo kama mali yao, bali kama mahali pa kuweza kulima na kujipatia mazao ya chakula kwa kulisha familia nzima na jamaa waliowatembelea. Baba wa nyumba, alikuwa na madaraka ya kupangua utaratibu wa vipande vilivyokatwa; hasa pale alipoamua kuoa mke mwingine. Kawaida wake walitumia vipande vya ardhi walivyokatiwa kuvisimamia kama mali ya baadaye ya watoto wao wa kiume.



Picha: Mama na mtoto wakilima kwenye shamba wakitumia vijembe vidogo.

**Jamii ya Wachaga:**

Mfano mwingine ni ule wa Mkoa wa Kilimanjaro, sehemu ya Uru. Katika sehemu hii, ulimaji wa mazao ya chakula ulifanywa na wanawake. Kila mke katika nyumba alikuwa na kipande cha ardhi katika shamba la mume *kihamba*. Mwanamke aliwajibika kulima mazao ya kutosheleza haja ya familia na pia kutoa sehemu fulani kwa baba mwenye nyumba. Akina mama hao walipanda kunde, viazi na mboga za majani katika vipande vyao; na katika vipande vya akina baba kulipandwa ulezi. Hadi leo ulezi hutumiwa kupikia pombe aina ya *mbege*. Kipande cha ardhi cha baba kilishughulikiwa na familia nzima kwa ujumla ikiwa ni pamoja na baba mwenyewe, mke (wake) na watoto. Kwa pamoja walitayarisha shamba na kupanda ulezi. Kazi ya kuhamisha ulezi ilikuwa ya wanawake. Akina mama pia walishirikiana na waume zao katika kuhifadhi ulezi katika *kihenge* (ghala ya kuhifadhi chakula). Baada ya kuweka ulezi katika *kihenge,* mwanamke hakuwa na usemi juu ya matumizi yake. Ulezi wote ulihesabika kuwa ni mali ya baba.

Kutokana na mifano hii miwili, ni dhahiri kuwa, suala la akina mama na watoto halikutiliwa maanani ipasavyo. Hapa tunaona kwamba, mume alimnyonya mkewe (wakeze) kwani licha ya kuwakatia vipande vya ardhi na kuwataka walime mazao ya chakula kwa familia nzima katika vipande vyao, aliwataka pia wamfanyie kazi kwenye shamba lake. Mfumo huu wa kilimo, kwa hakika ulihusiana na unyonyaji kwa sababu wanawake hawakuwa na madaraka juu ya ardhi, wala kile walichovuna.

**Mfumo wa Umilikaji Ardhi katika Vijiji vya Ujamaa.**

Katika sheria ya kuanzisha vijiji vya Ujamaa, kijiji ambacho kimekubaliwa ndicho kina haki ya kumiliki ardhi ya eneo la kijiji. Kijiji cha Ujamaa katika madaraka yake ya kumiliki ardhi kinagawa ardhi katika utaratibu ufuatao.

Kwanza, eneo kiasi kadhaa hutengwa kama shamba la kijiji. Wanakijiji wote wake kwa waume wenye umri wa miaka 18 na kuendelea wanawajibika kufanya kazi katika shamba la kijiji kwa siku zilizokubaliwa katika wiki. Pili, shamba lisilopungua ekari mbili hugawiwa kila kaya. Mkuu wa kaya ni baba wa nyumba na ndiye ana uamuzi wa mwisho kuhusu sehemu ya ardhi ya kaya yake. Kwa kawaida nyumba ya kuishi hujengwa kwenye shamba la kaya. Kwenye shamba hili mazao ya chakula hulimwa.

Tatu, kuna mashamba ya bega kwa bega ambayo chini ya utaratibu wa mashamba hayo, hugawiwa kwa kila mtu. Kila mwanakijiji hukatiwa shamba lisilopungua ekari moja. Kila mtu anawajibika kutunza shamba lake na kuhakikisha kwamba kila mwaka linalimwa. Mavuno yatokanayo na shamba la bega kwa bega humilikiwa na mwenye shamba.



Picha: Wanakijiji, wake kwa waume, wakilima kwenye shamba la kijiji.

Kwa kiasi fulani, katika utaratibu huu wa kugawa ardhi katika vijiji vya Ujamaa. wanawake wana haki ya kutumia ardhi hasa chini ya mpango wa mashamba ya bega kwa bega. Hata hivyo, bado kuna walakini. Wanawake hawana uamuzi kuhusu ardhi iliyopangiwa kaya. Mathalani, itokeapo baba wa kaya akafariki, ardhi hiyo itatwaliwa na watoto wa kiume, kama ilivyo kimila. Hivyo inadhihirika hapa kwamba, sheria ya kimila inaendelezwa hata katika vijiji vya ujamaa.

**Haja ya Akina mama:**



Picha: Wanawake wakiwa wamebeba majembe mabegani huku wakiimba wakiwa wameinua mikono juu.

Akina mama sharti waelewe kwamba, kuna baadhi ya mila na desturi za kurithi ambazo huwanyima haki ya kumiliki ardhi pamoja na vitendea kazi vyake. Pia, mila na desturi hizi huwanyima uamuzi juu ya hata kile wanachokizalisha. Kwa hiyo, wanawake waelewe kuwa suala la haki ya akina mama kumiliki ardhi halijasawazishwa kwa kufuata misingi ya ujamaa. Chama na Serikali viangalie upya na kwa ukamilifu suala la akina mama kumiliki ardhi vijijini.

Yafuatayo ni madukuduku ya wanawake katika suala zima la kumiliki ardhi na masuala mengine yanayohusika na kilimo:

Kwanza, wapewe madaraka ya kutumia ardhi na kugawiwa kwa usawa pato linalopatikana kutokana na kilimo cha pamoja cha kaya.

Pili, Serikali na Chama vichunguze na kuchukua hatua za kufutilia mbali mila na desturi ambazo bado huwanyima wanawake haki ya kumiliki ardhi na uchumi waliochuma pamoja wakati walipoishi pamoja na waume zao.

Tatu, wanawake wakulima walioachika na wale ambao hawakuolewa wawe na haki ya kugawiwa ardhi bila kubaguliwa. Kuwepo pia na taratibu za kutendewa haki katika kugawa ardhi iwapo mwanamke ataachika au mume atafariki.

Nne, wanawake wapatiwe mikopo yenye riba nafuu ili nao waweze kununua mbegu bora, mbolea na zana za kazi za kisasa.

Tano, Chama na Serikali vielekeze mafunzo ya kipekee kwa akina mama vijijini kuhusiana na kilimo bora kwani wao ndio wazalishaji wakuu na ndio wanaoshiriki kwa ukamilifu katika utendaji.

Mwisho, mapinduzi ya kilimo vijijini yatategemea sana juhudi na maarifa ya wanawake kwani wao ndio wakulima wakuu. Ili kuwapa ari na motisha ya kuzalisha mazao zaidi, suala zima la umilikaji ardhi halina budi kutazamwa upya.

# SURA YA NNE

## HAKI YA WANAWAKE KUSHIRIKISHWA KATIKA UONGOZI

Kushirikishwa kwa wanawake katika uongozi na maendeleo yao ni jambo muhimu. Umuhimu huu unatokana na ukweli kwamba ili kuleta maendeleo ya watu, ni budi binadamu wote washirikishwe kwa ukamilifu katika kuyapanga maendeleo hayo. Hii inajumuisha uongozi wa pamoja katika shughuli zote zinazohusu mabadiliko katika maendeleo.

Hapa nchini petu, Serikali inatambua umuhimu huu wa kushirikishwa kwa wanawake katika uongozi na ujenzi wa ujamaa kwa ujumla. Hivyo, tangu uhuru, sera ya serikali kuhusu suala hili imetilia mkazo haki sawa katika nafasi za uongozi katika madaraka mbali mbali. Mathalani, kuundwa kwa vyombo vya kuwahusisha na kuwaunganisha wanawake kama Umoja wa Wanawake Tanzania (U.W.T.) ni jitihada za Chama na Serikali katika kutekeleza sera hiyo. Wajibu mkubwa wa Jumuiya ya U.W.T. ni:

(a) Kuwahusisha wanawake wa Tanzania ili fikra za kimapinduzi za Chama cha Mapinduzi juu ya Ujamaa na Kujitegemea na msimamo wa Chama juu ya ukombozi wa wanawake uweze kuwafikia na kueleweka kokote waliko.

(b) Kuwaongoza wanawake na kuwashirikisha katika shughuli mbalimbali za jamii, uchumi, maendeleo, ulinzi, utamaduni na mengineyo.

(c) Kujenga, kukuza na kudumisha hisia za kimapinduzi kwa wanawake wote na kupitia kwao ili kuwafikia watoto wote.

Kwa hiyo, U.W.T. kama chombo kinachotambulikana kitaifa, basi, kina wajibu wa kuwahamasisha wanawake ili

waweze kuingia katika uongozi wa ngazi zote na kushiriki katika maamuzi ya kimaendeleo.

Kushirikishwa kwa wanawake katika uongozi hakuishii katika jumuiya yao tu, bali hata katika Chama na Serikali. Inapofikia nyakati za uchaguzi au kupiga kura, wanawake hupewa nafasi za kugombea uongozi. Vilevile kitaifa, wanawake wana haki ya kupata madaraka katika ngazi mbalimbali kama vile uwaziri, umeneja, sheria n.k. kwa kufuata ujuzi na msimamo walionao.

Katika ngazi ya kijiji pia wanawake wana haki ya kushirikishwa kwa ukamilifu katika ngazi mbalimbali za uongozi na maendeleo kijijini. Serikali ya kijiji na kamati zake za maendeleo zina jukumu kubwa la kutoa maamuzi mbalimbali ya kimaendeleo. Hivyo, kuwepo kwa washiriki wanawake katika kamati hizi ni muhimu kwa maendeleo ya kijiji.

## UTEKELEZAJI WA SERA YA KUSHIRIKISHWA KWA WANAWAKE KATIKA UONGOZI/MAENDELEO

Pamoja na kwamba Chama na Serikali vinatambua umuhimu wa wanawake kushirikishwa katika ngazi za uamuzi na utekelezaji wa kimaendeleo na hivyo jitihada zilizokwisha tajwa juu, bado kuna matatizo yanayojitokeza katika kufanikisha sera hii. Mathalani, kitaifa nafasi za madaraka kwa wanawake hazijawa nyingi kulinganisha na idadi ya wanawake nchini. Mara nyingi hali hii inatokana na sababu nyingi. Mojawapo kubwa ikiwa ni nafasi za elimu kwa wanawake ambazo ama hazijawa za kutosha au hazijaweza kuwapa wanawake wengi ujuzi unaohitajika katika nyadhifa mbalimbali za kimadaraka. Waaidha, hata wanawake nao mara nyingine huwa wagumu katika kujitokeza kushikilia madaraka. Hili hutokana na kutojiamini pamoja na kwamba mtazamo wa sehemu ya jamii haujageuka kuhusu nafasi ya mwanamke katika uongozi na maendeleo ya jamii kwa

ujumla. Ni budi pia, wanaume wabadili mtazamo wao na kuwakubali wanawake katika uongozi.

Halikadhalika, katika maendeleo vijijini, wanawake wamekuwa washiriki wakuu katika masuala ya kuendeleza uchumi, ulinzi, elimu na ustawi wa jamii kwa jumla. Hata hivyo, kushirikishwa kwao katika uongozi hakutoshi hivyo, maamuzi yanayohusu mipango na maendeleo yao bado ni madogo yakilinganishwa kiidadi au vinginevyo. Ni muhimu iwepo sera mahsusi inayowashirikisha wanawake katika kamati mbalimbali za maendeleo vijijini. Mathalani, kushiriki kwa wanawake katika uamuzi wa matumizi ya mapato na mipango ya fedha vijijini ni muhimu. Kamati ya fedha na mipango ni kamati muhimu ya kutekeleza maamuzi ya wanakijiji, lakini ni bahati mbaya kwamba wengi wa wanawake hawashirikishwi kwa ukamilifu katika Kamati hii ambayo huamua ni jinsi gani mapato ya uzalishaji yatumike. Hii inasababisha wanawake wengi vijijini kutotambua pato lao kwa kuwa wanaume hulishughulikia suala hili zaidi. Kutoshiriki kwa ukamilifu kwa wanawake katika kamati kama hii kunahusika zaidi na elimu wanawake waliyonayo na pia vikwazo vinavyotokana na mila na desturi zinazohusiana na uzalishaji na umilikaji wa mapato na matumizi yake. Kutokana na hali hii, panahitajika elimu ambayo itasaidia kuwapa mwanga wanawake na jamii nzima kwa jumla. Kwa mfano, elimu ambayo inaweza kumpa mwanamke uwezo wa kutambua haki aliyonayo katika suala zima la mapato na mpangilio wa matumizi yake kama mazungumzo yafuatayo yanavyoonyesha.

Bwana Songoro:

Mama Halima, mwaka huu tumepata mavuno mengi ya korosho. Natumaini nitapata fedha nyingi za kutosha.

Mama Halima:

Ni kweli, tutapata fedha nyingi za kutosha. Lakini sijui tutagawana vipi!

Bwana Songoro:

Kwani hizo fedha zikipatikana lazima tugawane? Hizo ni zangu mimi mwenye nyumba. Wewe nitakupa tu baada ya kutosheleza kwa matumizi yangu. Hata hivyo, siyo lazima upate.

Mama Halima:

Hee!! Mbona unasema hivyo? Hujui kwamba nilifanya bidii sana kuliangalia hilo shamba?

Bwana Songoro:

Pamoja na kufanya hivyo, uliliangalia shamba kwa kutimiza wajibu wa kuangalia mali ya mume wako.

Mama Halima:

Katu! Sikubaliani nawe mume wangu. Kama tulishirikiana kwenye kuzalisha, basi tushirikiane pia kwenye mapato!!!

Wanawake wengi hupenda kushiriki kutenda kazi. Wanapokuwa wameshiriki au kushirikishwa katika kazi yoyote, hujivunia kuona mapato ya kazi waliyoitenda. Katika kuwashirikisha wanawake kwenye maamuzi ya kamati inayohusiana na uuzaji wa mazao na uchumi kwa jumla, kutampa mwanamke uwezo si wa kushughulikia mazao shambani tu, bali hata katika kuyapeleka mazao hayo kwenye mauzo. Baada ya mauzo, mwanamke anaweza pia kushirikishwa katika kutunza mahesabu ya mauzo yake. Kitendo hiki kinaweza kumsaidia kufahamu juhudi yake au mchango wake katika taifa na familia, Kwani hata kifamilia mwanamke ana wajibu mkubwa wa kutekeleza kazi za kilimo na kuangalia mifugo. Hivyo, inambidi awe na haki ya kushirikishwa katika maamuzi yanayohusu uchaguzi wa mbegu bora na mifugo inayofaa.

Shughuli nyingine za kijiji ambazo wanawake wanastahili kushirikishwa katika maendeleo yake ni kuhusu viwanda vidogo vidogo katika kijiji. Shughuli hizi ni zile za ufinyanzi, uhunzi, ushonaji, ufugaji, ufumaji na uhifadhi wa

chakula. Wanawake wakiwa kama wataalamu katika nyanja hizi, wana haki pia ya kushirikishwa katika kuuza na kujua mapato yanayotokana na bidhaa za shughuli zao. Ni jambo la maendeleo kuona mwanamke anayejishughulisha na uzalishaji mali na vilevile akiwa ana uwezo juu ya kile anachokizalisha. Mazungumzo yafuatayo kati ya Mama Sabena na Bwana Kunene yanadhihirisha usemi huu:

Bwana Kunene:

Mama Sabena, naona unajishughulisha sana na kazi za uzalishaji. Sijui unafaidikaje.

Mama Sabena:

Ukweli ni kwamba mimi najihusisha na kusuka mikeka, kufinyanga vyungu na kulima mazao bustanini kwa ajili ya kuuza ili nipate fedha za matumizi.

Bwana Kunene:

Inaonekana una bidii sana katika kazi yako. Sasa sijui kati yako na baba, ni nani huhusika zaidi na mauzo.

Mama Sabena:

Bwana Kunene, kwa kuwa mimi ndiyo hushughulikia uzalishaji nina wajibika pia kushughulikia uuzaji wake. Bidhaa zangu zikiwa tayari, hutafuta mahali nitakapoweza kuziuza. Baada ya mauzo, hushauriana na baba Sabena kuhusu kiasi ambacho nimepata.

Bwana Kunene:

Je, mama Sabena, baada ya mauzo yako, hutumiaje mapato yako?

Mama Sabena:

Hutumia mapato yangu kwa matumizi mbalimbali ya familia yangu.

Wanawake pia wana haki ya kushirikishwa katika uongozi wa maendeleo ya ustawi wa jamii zao. Hii ni nyanja inayowahusu sana kimalezi, kiutamaduni na hata kielimu. Kwa hiyo, wanapaswa waishughulikie sana na wanufaike na matunda ya kusukuma mbele maendeleo yao. Vijijini kwa

mfano, kuna kamati ya kushughulikia elimu, utamaduni na ustawi wa jamii kwa ujumla. Kamati hii ambayo — kama ingekuwa inawashirikisha wanawake inavyotakiwa - ina jukumu kubwa la kuelekeza jitihada za kimaendeleo kwa watoto ambao ni taifa la kesho. Wanawake wengi vijijini wana majukumu ya kuona maendeleo ya vijana wa kike na wa kiume ambao hawajasoma na wale ambao wanasoma au wamemaliza masomo yao. Maadili ya kiutamaduni, kimazingira yakisaidiwa na vyombo mahsusi vya kitaifa kuhusu eneo hili, vingeweza kutoa misingi imara kwa jamii nzima. Mathalani, taasisi zinazohusika zingeweza kuendesha mafunzo mbalimbali yanayohusu somo la ustawi wa jamii ili wanawake na wanakijiji kwa jumla wanufaike.

Vilevile wanawake vijijini washirikishwe katika masuala yanayohusu elimu, ikiwa ni mojawapo ya majukumu yao katika malezi ya watoto, pamoja na kufahamu mazingira ya elimu yao. Wanawake wanastahili wajishughulishe hasa na maendeleo ya elimu ya watu wazima. Ili wanawake waweze kuzifahamu haki zao barabara, hawana budi kupatiwa elimu ya kutosha, kwani itawasaidia kufahamu baadhi ya taaluma zilizoandaliwa kimaandishi. Mfano ni taaluma zinazoweza kupatikana kwenye kitabu cha *Ndoa na Talaka* kilichoandikwa na Y. Mwakasendo au kile cha *Sheria na Haki katika Ndoa* kilichoandikwa na E. Munuo.

Kushiriki kwa wanawake katika maendeleo ya elimu katika jamii, kushirikishwa kwao kwa ukamilifu katika maamuzi yanayohusu maendeleo ya elimu hiyo. Kwa mfano, vijijini wanawake wana haki ya kutoa maelekezo muhimu kuhusu elimu na vyombo vinavyohusiana na maendeleo ya jamii. Maelekezo hayo yanaweza kuwa yamelengwa kwenye shule za chekechea, elimu ya msingi, kisomo cha watu wazima na hata kwenye miradi ya kielimu na kampeni za kitaifa. Hali hii itaruhusu wanawake kijijini kunufaika na maadili ya maendeleo.

Katika kuongelea vipingamizi vya kumshirikisha

mwanamke katika uongozi na maendeleo yake kwa jumla, tumeona umuhimu wa kutolewa kwa elimu mahsusi itakayoweza kumfahamisha maadili ya haki zake. Kwa mfano, jumuiya ya U.W.T. ikishirikiana na vyombo vya kielimu nchini, vingeweza kuendesha semina za kuwapa nafasi wanawake wengi vijijini kuelewa haki zinazowakabili.

Elimu ya ukombozi itakayowawezesha kuondokana na mila na desturi za kikale ambazo zimekuwa zikiwaweka wanawake katika hali ya nyuma, ya kunyonywa na kupuuzwa kielimu, kiuongozi na kiutamaduni inahitajika katika jamii nzima kwa jumla. Elimu ya namna hii itauwezesha umma wa Kitanzania kuwa na binadamu walio na haki sawa katika ujenzi wa taifa lao.

## SURA YA TANO

### HAKI ZA WANAWAKE KATIKA MALEZI

Ni jambo muhimu kutambua kwamba mwanamke ana haki katika malezi ya watoto na jamii kwa jumla. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, kwa kuwa watoto wanazaliwa na mwanamke na mwanamume, basi watu hawa wawili wana haki sawa kwa watoto. Mara nyingi jamii imeamini kwamba watoto ni wa mwanamume tu — jambo ambalo humfanya mwanamke kukosa haki sawa juu ya maamuzi muhimu yanayohusu malezi ya watoto.

Kutokana na kuwa na haki sawa, wazazi wote pia wana wajibu sawa katika kuwatunza, kuwalea, kuwaelimisha na kadhalika.

Hali halisi ilivyo katika jamii yetu, mwanamke amekuwa akibeba mzigo mkubwa zaidi katika malezi ya watoto na familia lakini wakati huohuo akionekana kama hana haki juu ya watoto hawa kwa kuwa yeye ameolewa. Mathalani, mwanamke amekuwa akibeba mimba. kulea na kufanya shughuli zote zinazohusu kukua kwa mtoto akipewa msaada mdogo kutoka kwa mwanamume, na wakati mwingine akiwa ananyimwa haki ya kushiriki katika masuala muhimu ya watoto na jamii kwa ujumla.

Mara nyingi ndoa inapovunjika, sheria iliyopo haimpi mwanamke haki sawa ya kuhodhi (kumiliki) watoto. Sheria ya kiserikali na hata za kimila zimempa baba uwezo mkubwa zaidi wa kuhodhi watoto hasa wanaozidi umri wa miaka saba. Mwanamke angefanyiwa haki zaidi kama angepewa nafasi ya kuchagua kuishi na watoto au kuwa na uwezo mkubwa zaidi juu yao hata baada ya ndoa kuvunjika.

Aidha, wakati wa kifo cha mume, mila za makabila mengi katika jamii yetu hazimpi mjane haki na kuendelea kuwa na uwezo mkubwa kwa watoto. Mara nyingi, mila hizi

humwekea masharti magumu mjane endapo angependa kuendelea kuishi na watoto wake. Mathalani, kupewa uchaguzi au wa 'kurithiwa' katika familia ile na kwa hali hiyo kubaki na watoto — au kurudi kwao bila ya watoto wake. Hali kama hii inamnyima mwanamke haki ya malezi ya watoto hasa iwapo atachagua kurudi kwao. Kimsingi, hali hii ingerekebishwa ili pindi mzazi mmoja anapofariki, mzazi aliyebaki awe na haki ya kuhodhi watoto na kuendelea kuishi nao. Kama mwanamke ndiye mzazi aliye hai, ndugu wa pande zote mbili wanapaswa kumsaidia kulea watoto kwa sababu watoto ni jamii nzima.

Halikadhalika, watoto wanaozaliwa na mwanamke ambaye hakuolewa, kimila inachukuliwa kuwa watoto hawa ni wa ukoo wake na hivyo kuwapa babu au wajomba zao madaraka makubwa zaidi juu ya watoto hao. Ingawaje hakuna sheria mahsusi kuhusu kipengele hiki, mwanamke kama mzazi na mlezi mkuu angetendewa haki kama angepewa uwezo zaidi juu ya watoto wake. Mathalani, wakati wa kutoa maamuzi muhimu kuhusu elimu, ndoa, n.k. mwanamke huyu angekuwa na haki ya kutoa kauli ya mwisho, kwa kuwa yeye ndiye anayekaa na watoto na anajua zaidi tabia zao.

## MATATIZO YANAYOATHIRI HAKI ZA MWANAMKE KATIKA MALEZI

Katika jamii yetu, kumekuwa na vikwazo vingi vinavyoweza kumnyima mwanamke haki zake katika malezi ya watoto na familia kwa ujumla. Mila na desturi za jamii zetu nyingi bado ni kikwazo kikubwa katika suala hili. Kwa mfano, katika familia nyingi mwanamke hana usemi juu ya watoto wangapi wazaliwe kwenye ndoa na jinsi watakavyolelewa. Makabila mengi bado yanapendelea kuwepo kwa watoto wengi katika familia kwa sababu labda watoto wa kwanza wanaongozana wa kike tu, hivyo wangependelea wa kiume kwa ajili ya urithi. Mintarafu ya


hayo, wengine hupendelea watoto wengi wa kike ili wapate mahari kwa wingi. Katika hali hii, kuzaa kwa mwanamke bado kunatawaliwa zaidi na matakwa ya mwanaume au mtazamo na jamii.

Halikadhalika, watoto wamekuwa wakiazimiwa kuwa kama amana ya baadaye. Katika hali hii, wengi hujali zaidi idadi badala ya matunzo. Hali hii inamnyima mwanamke haki ya kutumia vyombo vinavyohusika kama Uzazi na Malezi Bora Tanzania (UMATI) ili aweze kupata idadi ya watoto anaotaka na atakaoweza kuwalea vizuri.

Aghalabu, kutolewa kwa mahari wakati wa ndoa kumekuwa na athari ya kumuona mwanamke hana haki na majukumu mbalimbali juu ya malezi ya watoto na familia kwa jumla. Kutokana na mwanamke kuolewa kwa mahari, watoto wamechukuliwa kuwa ni 'mali' ya upande wa mwanaume tu na hivyo kumnyima mwanamke haki ya kuwa na usemi juu ya maamuzi muhimu kwa watoto ambao yeye pia amewazaa.

Vile vile, mwanamke amekuwa akitarajiwa kuchukua jukumu kubwa zaidi katika kushughulikia malezi ya watoto na familia kuliko mwanaume. Mathalani, kutunza watoto, kazi za ndani, kuangalia afya zao pamoja na shughuli nyingine za nyumbani na kuzalisha mali. Licha ya hali hii ya kumchosha, mama, hutazamiwa pia kutoa mchango wake kwa jamii kama watu wengine.

Suala la uwezo wa mwanamke kiuchumi, linakuwa pia ni kikwazo kikubwa katika kumpa mwanamke haki sawa katika malezi ya watoto. Kutokana na ukosefu wa elimu, mazingira au mpangilio wa jamii, kiutamaduni, mwanamke amekuwa nyuma kiuchumi, jambo ambalo limemfanya aonekane kushindwa au asiweze kumudu malezi. Hata kama kimila angeachiwa watoto baada ya ndoa kuvunjika au kufiwa na mume, mwanamke huyu angekabiliwa na tatizo la kukubali hali hiyo endapo hatakuwa na msingi mzuri kiuchumi. Hata



Kazi nyingi za kuchosha hufanywa na mwanamke bila ya kujali afya na wakati wake.

kuwaweka watoto chini ya ukoo wa babu mjomba kwa mwanamke asiyeolewa kunaweza kuwa kumeathiriwa na mwanamke kutokuwa na sehemu au mali anayoweza kusema ni yake binafsi.

Matatizo yanayojitokeza yanaweza yakachukua muda kutatuliwa kutokana na ukweli kwamba, mgeuko wa kijamii, husus a upande wa utamaduni, haugeuki kwa siku moja. Lakini ili kuweza kusaidia katika kuharakisha mabadiliko hayo, wanawake wakisaidiwa na vyombo vinavyohusika vya kielimu na kiutamaduni vingechukua jukumu la kuzidi kuelimisha umma juu ya umuhimu wa malezi bora kwa taifa, haki na majukumu ya mwanamke katika malezi na hata masuala mengine yanayohusu malezi. Mafunzo haya

yanaweza kuwa kwa njia ya kuendesha semina, kutoa makala mbalimbali kimaandishi, kubadilishana mawazo na kushirikishwa katika mambo yatakayoendeleza kustawi kwa jamii.

==== **MWISHO** ====